TANGAZO LA SERIKALI NA. 403 la tarehe 24/5/2024

SHERIA YA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA,
(SURA YA 306)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 165)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA KUHUSU USAJILI WA LAINI ZA SIMU ZA MWAKA 2024

Jina

TS Na. 60 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Kuhusu Usajili wa Laini za Simu za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Kuhusu Usajili wa Laini za Simu, 2023 ambazo zitarejewa humu kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya jumla

2. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta neno "mdiplomasia" popote linapojitokeza katika Kanuni kuu na badala yake kuweka neno "mwanadiplomasia".

Marekebisho ya kanuni ya 10

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 10 kwa kufuta aya (a) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

"(a) mzazi au mlezi atawasilisha picha ya mtoto husika pamoja na mojawapo kati ya-
(i) nakala iliyothibitishwa ya cheti cha kuzaliwa cha mtoto au cheti cha kuasiliwa mtoto; au
(ii) hati ya kusafiria;".

Marekebisho ya kanuni ya 37

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 37 kwa kufuta kanuni ndogo ya (6) na badala yake kuweka kanuni ndogo ifuatayo:

Sura ya 306

"(6) Mtu ambaye anakiuka kanuni hii anatenda kosa chini ya Sehemu ndogo (b) ya Sehemu ya IV ya Sheria.".

Dodoma,
7 Mei, 2024

NAPE MOSES NNAUYE
*Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari*